

Chuo Kikuu cha Oregon
Kitengo cha Timu ya Uongozi wa Usawa na Ushirikishaji
Taarifa kuhusu Maadili, Maono na Madhumuni

Hapa chini utapata taarifa kutuhusu sisi, maono ya pamoja ya timu yetu kwa ajili ya kazi tunayofanya tukiwa wataalamu wa DEI na madhumuni yanayohuisha kazi na fikira za pamoja. Taarifa hii ni uakisi wa maadili binafsi kama tunavyonua kuyatekeleza katika utendaji wetu wa taaluma.

UONGOZI WA DEI: KUTUHUSU SISI

Sisi ni timu inayojali na yenye ubunifu inayofanya kazi ili kukuza mahusiano, kujenga uwezo wa asasi kwa ajili ya mabadiliko ya mageuzi na kuhimiza matendo ya upendo, uhalisi, ujasiri, uelewa, werevu na haki kwenye Chuo Kikuu cha Oregon.

MAONO YA TIMU YA UONGZO WA DEI

Tunaona jamii ya Chuo Kikuu cha Oregon ambapo ufanisi na utambuzi vinakombolewa kutoka kwa kumilikiwa na wachache na kupatikana kwa wote;

Mahali ambapo kusema ukweli katika utafiti, ufunzaji, huduma na utungaji wa sera zetu unaruhusu urekebishaji na matendo ya sasa ya uamuzi binafsi na pia ujengaji wa jamii;

Mahali ambapo mabadiliko ya binafsi yanahusishwa kabisa na mahusiano bora na mifumo ya asasi, miundo, sera na desturi zenye usawa;

Mahali ambapo kila mwanafunzi anathaminiwa kwa werevu na utu alio nao na tunayeshirikiana kuimarisha tamaduni mbalimbali zinazoboresha uwezo wa wanafunzi kuchangia kwa haki kwenye jukwaa la kimataifa.

Mahali ambapo kazi ya mageuzi ya asasi inawahusishwa wote, lakini haswa kuongozwa kuendesha na wale waliowezeshwa zaidi—kwa njia rasmi na isiyor rasmi—kuendesha mabadiliko na

Mahali ambapo ushahidi halisi wa makundi yaliyotengwa yanatafutwa, kuthaminiwa na kujumuishwa ili kuendesha mabadiliko makubwa na endelevu lakini hayabebeshwi mzigo wa kufnaya kazi.

MADHUMUNI YA TIMU YA UONGOZI YA DEI

Madhumuni yetu ni kuwesha ukombozi wa watu binafsi, mashirika na jamii kutoka kwenye mifumo, sera na fikra zinazozuia na kuficha. Tunanua kuchochea uvumbuzi, usawazishaji na ahadi ya usawa kupitia ufadhili wa masomo, ufunzaji, shughuli za ubunifu na ushirikishaji. Katika huduma kwa ajili ya dhamira ya masomo na haki, tunatambua na kuomba kurekebisha makosa ya asasi na kimfumo.